

# MAMLAKA

Tunamshukuru Bwana kwa vile alivyo na yale aliyoyatenda. Tukiweza tu kumfikiria hata tukiwa na mahitaji mbalimbali, yeze atatutimizia. Tusiwtazame watu, tusijitazame sisi wenyewe, tumtazame Mungu pekee. Tukimitazama yeze nguvu zake zitatujia katika maisha yetu, nyumba zetu, majirani wetu, majiji na jamii mbalimbali, janibu, mataifa na ulimwengu. Ikiwa watu wanasmamia wanachokijua ni ukweli na wanene jina, Yesu, nguvu za Mungu zingetembea. Ni rahisi jinsi hii.

## **Matokeo ya nguvu za Mungu.**

Nguvu za Mungu huanza kutembea tunaponena jina la Yesu. Hata hivyo huwezi kuziona nguvu za Mungu; utayaona matokeo ya nguvu hizi. Aghalabu watu huanguka chini ya upako wa Mungu katika mikutano yetu. Tunaona uponyaji wiki baada ya wiki. Lakini hatuoni nguvu za Mungu zikitujia. Tunaona matokeo yake.

Saratani, ugonjwa wa moyo, magonjwa ya neva na magonjwa ya ngozi huondolewa. Masikio hufunguka, macho huanza kuona, miguu isioweza kutembea huanza kutembea. Athari za kiharuisi zinasitishwa katika jina la Yesu. Miyo hupona na hufanya kazi tena. Ndoa na hisia hupona. Litaje tumelionia.

Hata hivyo, kufikia wakati huu, sijawahi kumwona Yesu. Niliwaza wakati mmoja kuwa ningetaka Yesu aje, aingie katika chumba changu, aketi na aongee nami. Hakuja vile nilivytarajia. Aliniuliza, "Mwanangu, uliningoja nije niingie chumbani, niketi na niongee nawe, sivyo?" Nikamjibu "Ndio" Aliendelea, "Sitafanya hivyo." Kwa majuma mawili nimekuwa nikijaribu kukwambia jambo unalohitaji kulisikia" Nilijua katika moyo wangu jambo ambalo yesu alitaka nilisikie, lakini nilitarajia Yesu aingie kwa njia fulani. Nilijua vizuri neno la Mungu linasema, "Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina lake, naye yupo hapo katikati yao, lakini sihitaji kumwona. Nikimwona, utukufu kwa Mungu, nitafurahia; na ukimwona, utukufu kwa Mungu nitafurahia pamoa nave. Lakini neno la Mungu linasema yuko hapa. Ikiwa watu wanangojea kuona matokeo kabla ya kuliamini neno la Mungu, hawatayaona matokeo hayo. Ni lazima tumwamini Mungu na neno lake kisha tuone. Muda baada ya muda tumeyaona matokeo kwa sababu tumeliamini neno la Mungu.

*Tomaso alisema, "Nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole changu mahali pa misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo."* Ninaamini kuna watu ulimwengu huu wanaofanana na Tomaso (na nilikuwa mmoja wao) ambao lazima waone kitu kabla ya kuamini. Yesu akamwambia Tomaso, "*Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono uutie ubavuni mwangu,*" Yesu aliendelea, "*Tomaso, wa heri wale wasioona, wakasadiki*" hawa ndio wamebarikiwa. Watayaona matokeo kila wakati.

## **Juu na kuinuliwa juu.**

Watu wa Mungu hawana budi kujua namna ya kumchochea Roho wa Mungu ndani yao kwa sababu sio kila wakati wamo mahali ambamo nguvu za Mungu zitatembua. Tunachochea kipawa hiki kwa kuangazia Yesu Kristo kikamilifu. Msawiri Yesu akiwa juu na ameinuliwa juu.... katika taswira. Msawiri akichomoza pale mawinguni. Yeye anachomoza juu na kuinuliwa juu. Tunapokuwa katika Mungu hatujitazami tena kama binadamu wa kawaida tu kwa maana neno linasema kuwa bali wote waliompokea Yesu, aliwapa uwezo kufanyika wana wa Mungu, ndio wale waaminio jina lake,

walozaliwa, si kwa damu, wala mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, mbali kwa Mungu. Sisi sio tena binadamu wa kawaida tu kwa sababu sisi ni watoto wa Mungu aliye juu sana. Yule Mungu aliye juu na aliyeinuliwa huishi ndani yetu. Sisi watu wake kama neno lituambiavyo tunahitaji kujikweka mahali Bwana wetu Yesu Kristo ametuweka. Hatuchukui nafasi ya chini, tukiwa maskini na wenyе dhambi wasio na matumaini lakini tumeketishwa pamoja na Kristo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo. Neno halisemi kwamba tumeketishwa katika ulimwengu huu. (Waefeso 2:6).

*“Basi mkiwa mmeifufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko.”* (Wakolosai 3:1) Yafikirini kuhusu yale yaliyo juu Kristo aishipo katika utukufu na umemetufu kwa sababu sisi pia tumeinuliwa pamoja naye.

Ikiwa tutafanya hivyo kila siku, majoribu yoyote tutakayokutana nayo, tutaweza kujiona pamoja na Kristo, tukiwa juu na kuinuliwa juu, tukizitazama chini hali zetu ngumu zilizoonekana kutushinda. Hazina nguvu dhidi yetu tena kwa sababu sisi ni watoto wa Mungu walionunuliwa kwa damu ya Yesu. Sisi ni zaidi ya washindi kwa Yesu Kristo aliyetupenda. Hivi ndivyo neno la Mungu hutuambia. Watu hufinyika na kushindwa kwa sababu hawajioni wakiwa juu na kuinuliwa juu pamoja na Bwana Yesu Kristo.

Hivi ndivyo mimi husema. “Wewe ndiwe uzima wangu na chemichemi ya nuru. Wewe ndiwe mwokozi. Wewe ndiwe chemichemi yangu ya kila baraka. Uko mawazoni mwangu na moyoni mwangu....” Nena jina la Yesu, sema, “Nakushukuru Yesu, nakusifu Yesu, nakupenda Yesu, nakuheshimu Bwana, wewe u juu na umeinuliwa juu. Umetukuka katika adhama yako yote. Wewe unawajibika kuniinua juu ili mimi pia niwe juu na kuinuliwa juu. Mimi ni zaidi ya mshindi ndani yako, Yesu Bwana wangu, ninapokuangazia wewe na nguvu zako na uwezo..... wa kuniinua juu pamoja nawe.

### **Pokea kile alichotukarimia**

Angalia, sio kwamba, lazima tujaribu kuwa wakristo na sio lazima tujaribu kuacha hiki au kile. Jambo hili halihusiani hata kidogo nasi kuuacha kufanya jambo lolote lile. Linahusiana na ukweli kuwa Mungu katika upendo wake katika Yesu ametufanya kila kitu. Linalotupasa kufanya ni kutambua alilolifanya na kupokea alilotukarimia.

Roho wa Mungu anahudumu kwa nguvu sana siku hizi za mwisho kuhusu utakatifu. Hatuwezi kutarajia kupokea uponyaji ikiwa tunazungukazunguka tukiitia unajisi miili yetu (mahekalu) au kufanya mambo yatakayolitia unajisi hekalu la Mungu. Kama tujuavyo kuna wakati ufikapo ambapo unasema, “Sitaki kumuasi Mungu, nataka kuacha uvutaji. Nataka kuacha ulevi. Nataka kuacha ulafi.”

Kwa kweli Mungu anajua sitakiwi kufanya hivyo. Yesu amenifanyia hivyo tayari, ninatakiwa tu kusema, “Baba nisamehe kwa kukuasi na kuliasi neno lako.” Hebu nikwambie hivi hili ndilo jambo rahisi sana katika ulimwengu huu kusema ikiwa hakika unataka kuwa huru; “Baba nisamehe.” kisha amini uwezo na nguvu zake kutembea ndani yako na kukomesha kila kikusumbuacho. Tunazungumuza kuhusu nguvu za Roho wa Mungu. Ni rahisi hivyo. Hata hivyo naendelea kuwaza kuwa sina budi kuufanya hivyo, lazima nifanye hivyo kwa hakika, sina uwezo wa kufanya lolote peke yangu. Nitashindwa. Hii nguvu ya fikra kutaka kutenda haifanyi kazi rafiki yangu. Ni kutaka kufanya kitu siku moja lakini siku inayofuata hakika. Ikiwa tutainuka katika mamlaka, hatutakuwa wafungwa tena.

Mamlaka ni nini? Mamlaka ni kuwa na uweza au enzi (amri) na nguvu. Yesu ametuinua na kutuweka katika nafasi hiyo. Ikiwa tutayachukua mamlaka, enzi (amri) na nguvu hatuwezi kuvuta tena maishani mwetu. Hatuwezi pia kunywa chochote ambacho hakimfurahishi Mungu.

Kwa nini ? Kwa sababu tayari tuko huru. Ikiwa tutawaelezea watu chochote, tuwaeleze kuwa yesu Kristo ametuweka huru. Yote haya yametimizwa. Ilifanyika pale msalabani. Damu ya Yesu imetuweka huru. Kile ninachotakiwa kufanya leo ni kulifahamu jambo hili. Natakiwa tu kuupokea uponyaji wangu na nisiendelee kufanya nilivyokuwa nikifanya.

Ni nini kitakachonifanya nianze? Kwanza, lazima njue kuwa kile ninachokifanya hakitokani na Mungu. Pili sina budi kusema, “ Baba katika jina la Yesu nisamehe kwa kukifanya.” Yohana 1:9 yasema kuwa damu yake Yesu, mwana wake, yatusafisha dhambi zote. Tukiziungama dhambi zetu, ye ye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote. Hivi ni kusema kuwa Mungu huniona kama sijawahi kufanya dhambi. Ameyashau hayo yote.

Mlango wa gereza umefunguliwa.

Ikiwa amesahau kuhusu yote niliyoyafanya, kwa nini niendelee kushikilia kuwa siwezi kuyaacha. Sina budi kuingia katika yale Mungu amenikarimia tayari na nguvu za Mungu zitanijia. Ikiwa moyo wangu umemwangazia Mungu, nguvu zake zitatemebea na huo ndio utakuwa mwisho wake..... na sitasumbuka kwa sababu nimeliacha jambo lile. Ahsante, Yesu. Mlango wa chumba cha gereza umefunguliwa wazi naketi pale na uamuzi rahisi. Nitatoka gerezani nikiwa huru, au nitaendelea kuketi pale mlango ule ukiwa wazi.

Wakati mmoja nilipokuwa nikimhudumia mwanamke mmoja, niliona tu kile nilichokuwa nikielezea. Niliona chumba kikiwa na paa na kuta pande zote. Mlango ulikuwa umefungwa wakati huo. Tulipoendelea kumwombea mwanamke huyu, mlango ulifunguka. (Bwana Yesu aliufungua mlango ule) nikamwambia, “Unatazama pande zote lakini mlango umefunguliwa. Uko wazi. Umeshinda ukiangalia dari, umeshinda ukiangalia pande, nyuma na sakafu lakini huangalii mlango. Kwa nini usitazame mlango?”

(Mlango ni nini?- Bwana Yesu mwenyewe na ameufungua mlango wa seli katika gereza.) nikasema, “Rafiki kwa nini usitambue tu ukweli na upitie kwenye mlango uupate uhuru wako?” aliniangalia kwa mshangao na kusema, “Sijawahi kujua kuwa nilikuwa huru.”

Unajua kwa nini? Kwa sababu alikuwa akiendelea kutazama juu pahali palipokuwa na vizuizi, akaendelea kutazama kuta, pahali palipokuwa na vizuizi, aliendelea kutazama nyuma palipokuwa na vizuizi, aliendelea kutazama sakafu( hapakuwa na njia ya kutokea pale.) Huyu mwanamke hakuwa na budi kumtambua Yesu na ukweli kuwa alikuwa huru katika Yesu na ajiedee zake.

Nashukuru Mungu kuwa mwanamke huyu aliweza kuelewa uhuru uliomo ndani ya Yesu. “sitaki kuendelea kuridhika katika hali hii ya upuuzi katika maisha yangu tena. Niko huru tayari!” Alisema kwa mshangao. Alikubali ndani yake kuwa alikuwa huru, nguvu za Mungu zilimjia, kisha uhuru ukaja lakini sio kabla.

Tukiachilia akili zetu kutawala maisha yetu, tutajikuta tukikosa kufaulu mara kwa mara. Lazima tugeuze na kufanya upya fahamu (akili) zetu kulingana na neno la Mungu. Neno la Mungu husema kwamba tuna mamlaka juu ya vitu vyote.

Bwana anataka ujumbe huu ujulikane ili miujiza na uponyaji ziendolee kuongezeka katika siku zizazo. Miujiza na uponyaji hazitazidi tu makanisani bali pia katika nyumba zetu. Nguvu za Mungu zitazidi kuongezeka.

### **Utakatifu wahitajika.**

1 Wakorintho 6:9-10 yasema kuwa watu wasio haki (wadhalimu) hawataurithi ufalme wa Mungu. *Neno linasema msidanganyike. Watu wanaofanya mambo yafuatayo hawataurithi ufalme wa Mungu isipokuwa wabadilike: waasherati, waabudu sanamu, wazinzi, wafiraji, walawiti, wevi, walafi, watukanaji na wanyanganyi.*

Hakuna ambaye angekuwa na uzima katika Mungu isipokuwa Yesu alilipa gharama ya dhambi zetu. Kwa sababu alitupenda, alikuja na kumwaga damu yake msalabani na kulipa gharama..... Yesu alifungua wazi milango ya seli za gereza. Alisema, “Njooni kwangu nyinyi nyote msumbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Nitampa uzima. Mimi ndimi njia, na kweli na uzima; mtu haji kwa Baba ila ni kwa njia ya mimi. Mimi ndimi mlango. Pitia kwenye mlango uingie katika uzima, afya, kukarimiwa kwa kiungu, ulinzi na baraka za kila aina.

(1 Wakorontho 6 inaendelea kusema, “*Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii.*” “Mlikuwa” ni njeo inayoonyesha wakati uliopita. Wakati tulimpokea Yesu miyoni mwetu kama Bwana na mwokozi, nguvu za shetani na mambo yetu ya kimwili ziliondolewa kutoka maisha yetu (tukielewa au la) tuliwekwa huru wakati ule na tuko huru sasa. Kwa hivyo sasa ni wakati wa kuziondoa taka.

“*Lakini mlioshwa kwa neno la Mungu, kwa damu ya Yesu*” humaanisha kuwa hakuna chembe ya kitu chochote kile ndani yetu kisichotokana na Bwana tena. Mungu mwenyewe ametuosha na kutufanya safi. Ni jukumu letu kudumisha usafi huu. Mungu anafanya kazi ndani yetu na kwa sisi, akituwezesha kuifanya. Wakati tunapoutambua ukweli huu tutaona kuwa hakuna chochote kitakachotuzuia tena.

“Mlitakaswa” humaanisha mmefanywa watakatifu na Mungu tayari amewafanya watakatifu. Je, unajiona ukiwa mtakatifu au bado unajitazama kama mwenye dhambi aliye maskini, mkosa tumaini na mshinde?. Biblia yasema kuwa kuitia damu ya Yesu sisi hatuonekani tena kama wenyewe dhambi. Sisi ni haki ya Mungu katika Kristo..... Tumetakaswa, tumefanywa watakatifu kwa damu yenyе thamani ya Yesu. Sisi ni mzao mteule, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu.

### **Jinsi tunavyotakiwa kujiona**

Yesu ndiye mzaliwa wa kwanza wa wale waliokufa nasi tunamfuata nyuma. Tumeinuliwa. Lazima tujione vile. Ikiwa tutajiona kama viluwiluwi katika uchafu, hatutaweza kuinuka kamwe. Hatutaweza kuinuka na kuona yale yote Mungu ametufanya tayari. Sisi ni wana wa kiume na wakike wa Mungu aliye juu sana waliovishwa mavazi meupe. Utukufu wa Mungu u ndani yetu. Sisi ni mahekalu ya Mungu aishiye.

Tukikosa kuanza kujiona jinsi hii, tutakuwa tumekosa shabaha ya habari njema ya Yesu Kristo na upendo wa Mungu. Ametuweka huru tayari na tunachotakiwa kufanya ni kupokea tu. Nina thamani kwa kuwa Yesu amenifanya kuwa na thamani. Nimetakasika kwa sababu Yesu amenitakasa. Nimependwa kwa sababu Bwana amenipenda.

Kuwa na mamlaka kunamaanisha kwamba nina nguvu katika mbingu na nchi, katika jina la Yesu kwa sababu Yesu amenipa, mamlaka, nguvu na uwezo juu ya kila kitu.

1 Wakorintho 6:11 inaendelea, “*Lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo.*” Mungu anatuita wenyе haki. Ikiwa Mungu anatuita hivyo tumemwomba msamaha, sisi ni kina nani twendelee kujiona kama wasio haki? (Warumi 8:29) Nani awezaye kusimama dhidi yangu na kusema mimi ni mwenye dhambi? Shetani mwenyewe ndiye huwashtaki ndugu na hana kibali cha kunishtakia kifo. Itakuwa uongo kwa sababu Yesu ameniweka huru. Yesu amekuweka huru. Sema, “Yesu ameniweka huru kutokana na sheria ya dhambi na kifo, magonjwa na ufukara. Mimi ni huru kabisa. Nashukuru Yesu”.

Sina budi kuanza kujiona jinsi Mungu anavyoniona. Kwa nini nijione kama kiluwiluwi asiye na thamani wakati Mungu anaponiona nikiwa juu na nimeinuliwa juu? Kuna anayedanganya mahali fulani. Hebu nikuambie, sio Mungu, huenda najidanganya mwenyewe au ninauamini uongo wa shetani.. udanganyifu huu huiendelea kunionyesha kuwa mimi sina thamani, niko chini, aliyeumbuliwa, asiye thamani, awezaye kuyapata magonjwa ovyo, na mtu aliyeshindwa kabisa.

Huu ni wakati unapotakiwa kuanza kumsikiza Mungu. Ni kitu kimoja kusema, “Ndio nitamsikiza Mungu” ukifanya hivyo hakika basi utasikiza vile neno lake lisemavyo na sio kusikiza tu. Wakati Biblia inasema “ Shika” inamaanisha usikize kwa bidii na kutenda.

Sisi tuko juu na kuinuliwa pamoja na Bwana Yesu, sisi tutawahukumu malaika na ulimwengu siku hiyo ya mwisho. (1Wakorintho 6:1-2) Kwa wakati huu tusiwhukumu wasioamini tuwapende. Jambo hili ni muhimu sana. Tunatakiwa kukumbuka jinsi tulivyokuwa kabla ya Bwana Yesu kuyagusa maisha yetu kwa upendo wake na kutuweka huru.

Wasioamini bado wamo utumwani kwa sababu hawajaona kuwa mlango umefunguliwa wazi. Yesu amesimama pale mlangoni akisema, “Njoo, Njoo kwenye uhuru. Njoo kwenye uzima. Njoo kwenye afya. Njoo kwenye kukarimiwa kiungu na baraka za kila aina”. Mlango umefunguliwa wazi hata kwa wasioamini. Mlango wa gereza umeondolewa na Bwana Yesu Kristo, naye sasa amesimama pale kama mlango wa uzima. Tazama ni rahisi sana. Toka nje katika jina la Yesu.

### **Sio chini ya nguvu zozote.**

*Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya juwezo wa kitu chochote.* (1 Wakorintho 6:12)

Kwa nini nisitiwe chini ya uwezo wa kitu chochote?. Kwa sababu Mungu ameniweka huru kutokana na nguvu za shetani, kutokana na nguvu za magonjwa, maradhi na umasikini katika ulimwengu huu na nguvu za mwili wangu. Hivyo ni sawa. Niko huru kuishi kama mwenye haki na mtoto mtakatifu wa Mungu anayesimama sawa sawa na babake aliye juu sana. Mungu anajua kuwa ikiwa kuna kingine chochote ambacho kina nguvu dhidi ya maisha yangu basi nimekiachilia mimi kichukue mamlaka juu yangu. Je, umelewa hivyo? Ninatakiwa kuwa na nguvu juu ya kila kitu. Hakuna kinachotakiwa kuwa na nguvu juu yangu isipokuwa Roho wa Mungu. Paulo alisisitiza jambo hili kwa Wakorintho aliposema, “*Ninakataa kuwekwa chini ya uwezo wa kitu chochote,*”

Mimi ni mtu aliye huru na nakataa kufungwa kwa chochote isipokuwa Roho wa Mungu. Ikiwa nimekosea, Mungu hanitishi. Humtii Mungu nikiwa huru. Ni huru kumpenda Mungu kwa maana alinipenda kwanza.

Tazama Mwanzo 1:26-31 Neno linasema kuwa Bwana Mungu aliumba mwanadamu kwa mfano wake kisha akampa Adamu mamlaka juu ya nchi na vyote viishivyo. Mungu alitupatia mamlaka juu ya kila kitu pia. Alitupatia haki ya kuzitawala hali (kuliko kutawaliwa na hali) katika jina la Yesu Kristo.

### Zaidi ya washindi ndani ya Yesu Kristo

Ikiwa nimepata kuelewa mamlaka basi ningeanza kuwa mmoja wa washindi katika Yesu Kristo, ningejua kuwa mambo yangeenda vile Mungu amesema yangeenda kuliko vile shetani anasema yangeenda. Watu wengi wa Mungu hawajalisikiza neno la Mungu katika sehemu hii na wanashindwa kila wakati. Wanafikiria kuwa wao ni wanyonge na wametamauka- kuwa hakuna chochote kinachoweza kuwatendekea.

Tazama Zaburi nane.

- “*Wewe, Mungu, Bwana wetu (tutamsifu hapa) jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote! Wewe umeuweka utukufu wako mbinguni*
- *Utukufu wa Mungu hutujaa. Hii inamaanisha kuwa tumewekwa juu ya mbingu, pia kulingana na pale tulipo au haki zetu kama wana wa Mungu aliye juu sana. Tumepewa mamlaka.*

“*Vinywani mwa watoto wachanga na wanyonyao umeiweka misingi ya nguvu kwa sababu ya wanaoshindana nawe; uwakomeshe adui na mijilipiza kisasi*”

Mungu huwasitisha maadui. Niko huru kufurahi, kuwa Mungu hupigana vita vyangu.

- *Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota ulizoziratibisha, mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie?*

Kwa maneno mengi binadamu anamuuliza Mungu kwa nini anajishugulisha naye. Mimi ni kitu gani hata uje uniangularie. Tunalazimika tuanze kumwona binadamu jinsi Mungu anavyomwona.

- “*Umemfanya mdogo punde kuliko malaika umemvika taji ya utukufu na heshima.*”

Binadamu amefanywa mdogo kuliko malaika lakini amevikwa taji ya utukufu na heshima. Tunatambua kwamba Yesu yu juu ya malaika katika Waembrania sura 1 na 2. Kwa sababu ya kile Yesu alitufanya msalabani kupitia kwa damu yake, sisi tuliokuwa tumetengwa na Mungu, sasa tumerejeshwa pahali ambapo Adamu alikuwa kabla ya kumwondokea Mungu. Hivi ni kusema kuwa, binadamu yu juu kuliko malaika.

Malaika sio wana wa kiume na wa kike wa Mungu aliye juu sana. Malaika hawakuumbwa kwa mfano wa Mungu. Sisi tumeumbwa hivyo na kwa sababu ya kile damu ya Yesu ilitufanyia, tumeinuliwa mahali palipo juu kuliko kabla ya mtu kuanguka. Tunangojea kurudi kwa Bwana wetu Yesu tukifanya kazi yake kwa bidii wakati huu, tukingoja kumwona akija mawinguni. Miili yetu itageuzwa ghafla na Roho wa Mungu atatupatia miili mipya ambayo itadumu milele na Mungu. Namshukuru Yesu!

Lakini sasa miili yetu inayokufa ndio husheheni utukufu wa Mungu. Roho wa Mungu yu hai ndani yetu kwa sababu ya Yesu na kila tunachokiona ndani yake....

Zaburi 8 inaendelea.

- “*Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.*”

Hii inamaanisha mamlaka. Pia nguvu. Basi hutalemewa tena na Shetani au mashaka yako au nyama (miili yetu).

- “*Kondoo na ng'ombe wote pia; naam, na wanyama wa kondeni; ndege wa angani, na samaki wa baharini; na kila kipitacho njia za baharini. Tumepewa mamlaka juu yake. Wewe, Mungu, Bwana wetu jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!*”

Mungu amepanga iwe hivi ili tuwe na mamlaka juu ya kila kitu. Sisi ni zaidi ya washindi kwa Yseu Kristo. Yesu alikuwa mshindi na aliufungua mlango. Tu zaidi ya washindi kwa sabau tunaupata ushindi kutokana na kile alichokifanya. Hatukujikarimia ushindi huu. Hakika hatungeufanyia kazi kwa sababu Yesu pekee angelifanya hivyo. Namshukuru Mungu kila siku kwa sababu ya ukweli huu. Natakiwa tu kuutambua.

Sema, “Yesu, nakuajabia sana. Umeniokoa, umeniponya, umenikomboa, unanilinda na kunikarimia, umenifanya mtoto wa Mungu.” sikujitendea haya. Mungu katika upendo wake alinitendea na kile nilichohitaji kufanya ni kupokea tu na kufurahia na kushukuru kwa sabau yake.

Waefeso 1:18-23 inaonyesha Paulo akiliombea kanisa waweze kujuu ukuu wa uweza wa Mungu ndani yao. Zile nguvu zilizomfufua Kristo kutoka wafu na yuaishi ndani ya waaminio. Jina la Yesu limeinuliwa juu ya chochote kile. Yesu ndiye kichwa nasi mwili na kila kitu ki chini ya miguu yetu. Jambo hili linamaanisha tuko chini ya amri (uweza) ulinzi na uongozi wa Yesu Kristo. (Uweza) amri wote mbinguni na duniani ni wetu, mwili wa Kristo na jambo hili linamaanisha kuwa kila kitu kingine kiko chini ya miguu yetu. Hii humaanisha kuwa tuna uwezo juu ya chochote kile kisichotokana na Bwana. Watu wa Mungu wakielewa hivi, hakutakuwa na fadhaa au uovu katika maisha yao. Kuona kuwa tumewekwa huru kutokana na haya yote, sisi ndio tunaruhusu hali tulizo nazo. Tunaziruhusu tunapokosa kuchukua mamlaka, nguvu na uwezo juu yake.

“*Lakini kwa mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda , kwa yeye aliyetupenda. Mungu akiwa upande wetu, ni nani aliye juu yetu?*”(Warumi 8:29-37). Ikiwa Mungu ametuhesabia haki sisi ni kina nani (au yejote yule) kusema hatuko haki? Tu huru. Hakuna kitakachotutenganisha na upendo wa Mungu tulio nao katika yesu Kristo. Mungu ametupa mamlaka na uwezo katika jina lake. Kwa nini tusiutumie? Hatuwezi kutumia ikiwa hatujui kuwa tunazo

### **Chochote ukiombacho katika jina lake**

Hebu nikwaambie, juma baada ya juma, kwa Roho wa Mungu, tunachukua uwezo juu ya maradhi, magonjwa, umasikini, utasa au chochote kitokanacho na mwovu Shetani. Utaona tukiamrisha mambo haya yaondoke nayo huondoka. Lazima yaondoke katika jina la Yesu. Unapojuu katika moyo wako kuwa unaponena katika jina la Yesu, mambo yatafanyika, lazima yafanyike.

“*Amin, amin, nawaambieni, yeye aniaminie mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye (sisi)*

*atazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya mwana*” . (Yohana 14:12-14)

Nani anatakiwa kuomba na kuchukua amri? Sisi tunatakiwa. Neno hili “omba” si mwafaka katika matumizi yake. Neno hili linamaanisha “kudai” hatudai kutoka kwa Mungu, tunadai, “ Shetani, ondoa mikono yako kutoka kilicho cha Mungu, katika jina la Yesu!” Tunapofanya hivyo, Yesu anatenda. Iwapo tunatumikishwa katika nyanja fulani sisi si watumwa tena katika Yesu kwa sabau sisi tayari tumekuwa huru kutokana na utumwa huo. Tunatakiwa kutambua kuwa tu huru.

### **Kutoamini na mamlaka.**

Kwa nini tunawaona wengine kama wasioamini? Hakika wao si wasioamini kwa sababu damu ya Yesu tayari imetolewa kuwaokoa. Wao wanajifanya kuwa wasioamini. Kwa maneno mengine, watu tayari wameokoka machoni pa Mungu. Wanatakiwa kuingia katika wokovu huu na kuutambua.

Utukufu! wanatakiwa kusema, “Yesu Kristo, nakuhitaji, wewe ni Bwana wangu, ingia katika moyo wangu.” Wako huru tayari lakini hawajui. Wanakaa katika chumba cha gereza mlango ukiwa umefunguliwa wazi nao wakifanya mambo kivyao. Wakinyenyeka, nguvu za Mungu zitayajia maisha yao na watakuwa huru.

Wanafunzi walimuuliza Yesu, “Mbona sisi hatuwezi kumtoa pepo?” (Mathayo 17:20) Yesu akawajimbu, “Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu.” Alikuwa akiongea juu ya nani? Wamekuwa wakitoa pepo kila upande.... walikuwa wakifanya hivyo kila wakati. Lakini walikuwa wamesahau kuwa walikuwa na mamlaka (uweza) ambayo Yesu aliwapatia kutoka kwa Baba yake. Hawakuwa wakiyafanyiza kazi.

*Yesu akawaambia, “Hamngeweza kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. kwa maana, amin, amin, nawaambia, mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali, mtawambia milima huu. Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka, wala halitakuwako neno lisilovezekana kwenu!”*

Halitakuwako lisilovezekana kwenu, lakini lazima tuchukue hatamu. Hatuna budi kufanya kulingana na neno la Mungu na kutafanyika vile Mungu anavyosema katika jina la Yesu.

“Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu!” (Wafilipi 4:13) sina utukufu wowote binafsi. Nina uwezo wa Mungu katika Bwana Yesu. Utiifu wa neno la Mungu..... nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. Unaona? Nimepewa mamlaka na Bwana Mungu na sina budi kuyafanya kazi. Lazima nichukue mamlaka dhidi ya kila aina ya woga. Sina budi kuchuka mamlaka dhidi ya mashaka na fadhaa nani ataifanya kazi hii? Yesu.

Tunatakiwa kutambua kile Mungu amefanya. Ametuweka huru kutokana na mambo haya yote. Hivi ndivyo nasema, “Niko huru” siogopi tena. Woga ondoka sasa katika jina la Yesu. Mimi sitatamauka tena. Niko huru kutokana na kutamauka, katika jina la Yesu.

Katika Mathayo 28:18 Yesu alisema, “*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*” akaendelea kusema, “Basi enendeni” unga neno hili na Yohana 14 Basi enendeni..... na mfanye nini?

Mlifundishe neno la Mungu na habari njema kuhusu neno la Mungu katika Yesu. Mkawafanye mataifa yote wanafunzi, Alisema. Wafundisheni yote niliyowaamuru kama watu wangu. Nena katika jina la Yesu. Fanya kazi za Mungu ili apokee utukufu. Fufua wafu.

Katika Luka 10:19-20 Yesu alisema, “*Tazama nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.*”

Hii inamaanisha mamlaka. Wakati wa ukombozi wote ambao nimenafasika kuwa sehemu yake, sijawahi dhurika. Ahsante Yesu. Pepo hawa huwatoka watu kwa njia yoyote ile katika jina la Yesu.

Nilipokuwa nikihudumu wakati mmoja, mtu mmoja akiwa chini ya nguvu za pepo alijaribu kuzuia kazi ya Mungu. Alipaaza sauti, "Nimetumwa na shetani kuzuia mikutano hii. Rudini kwenye makanisa ambayo yamekufa na msahau kuhusu yale mnayoyahubiri!" kisha akasimama na kuniangalia usoni tayari kunipiga. Nguvu za Mungu zilimjia na akaanguka chini... na pepo wakamtoka. Katika jina la Yesu lazima yangetoka.

Hatupaswi kuogopa chochote kwa sababu tumepatiwa mamlaka. Tumepewa amri (uwezo). Tumepewa nguvu zote jinsi neno la Mungu linavyosema na tunatakiwa kuyaona mambo jinsi hii. Huu ni mlango juu ya chochote kile. Sio tu juu ya Shetani, bali pia amri (uweza) juu ya dunia yote, juu ya wanyama wote wa kondeni na kila kitu Mungu ametupatia mamlaka na nguvu juu yake. Ni mamlaka yake. Ni nguvu zake. Ni uweza wake tuupokee.

Tunayatumia jinsi gani? (jitayariske kutenda.) Tunayatumia katika jina la Yesu.

Kila wakati tunenapo jina la Yesu, tunatambua uwepo wake. Tunatambua uongozi wake. Tunatambua mamlaka yake juu yetu. Tunaposema Yesu ni Bwana, tunasema, "Bwana Yesu una mamlaka, nguvu na uweza (amri) juu ya maisha yangu. Nitafanya kile utakachoiniambia." Ninapoamrisha pepo waondoke hawana budi kuondoka katika jina la Yesu, magonjwa lazima yaondoke. Lazima yanitii. Kwa nini? Yesu yuaishi ndani yangu.

Wagalatia 2:20 yasema, "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, (weka jina lako hapo), bali ni Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu"

Uhai wangu si mali yangu tena. Uhai wako si mali yako tena tumenunuliwa kwa thamani. Neno mwisho ni mwa 1 Wakorintho 6 linasema, "Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu na roho zenu kwa maana ni za Mungu.

© 1985, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,  
all rights reserved, used by permission.

[www.gloritytogod.org](http://www.gloritytogod.org)